BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR 2016 - 2020

1.	**Mhe.**	**Zubeir Ali Maulid**	**-**	**SPIKA**
2.	**Mhe.**	**Mgeni Hassan Juma**	**-**	**Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake**
3.	**Mhe.**	**Shehe Hamad Mattar**	**-**	**Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni**
4.	**Mhe.**	**Mwanaasha Khamis Juma**	**-**	**Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani**
5.	**Mhe.**	**Balozi Seif Ali Iddi**	**-**	**MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda**
6.	**Mhe.**	**Issa Haji Ussi Gavu**	**-**	**MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka**
7.	**Mhe.**	**Haji Omar Kheri**	**-**	**MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu**
8.	**Mhe.**	**Haroun Ali Suleiman**	**-**	**MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi**

9.	**Mhe. Mohammed Aboud Mohammed**	**-**	**MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais /Uteuzi wa Rais**
10.	**Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed**	**-**	**MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge**
11.	**Mhe. Mahmoud Thabit Kombo**	**-**	**MBM/Waziri wa Habari, Utalii,**
			na Mambo ya Kale/Jimbo la Kiembesamaki
12.	**Mhe. Riziki Pembe Juma**	**-**	**MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake**
13.	**Mhe. Balozi Amina Salum Ali**	**-**	**MBM/Waziri wa Biashara, na Viwanda / Uteuzi wa Rais**
14.	**Mhe. Balozi Ali Abeid Karume**	**-**	**MBM/Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo/ Uteuzi wa Rais**
15.	**Mhe. Rashid Ali Juma**	**-**	**MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Amani**
16.	**Mhe. Hamad Rashid Mohamed**	**-**	**MBM/Waziri wa Afya / Uteuzi wa Rais**
17.	**Mhe. Maudline Cyrus Castico**	**-**	**MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais**
18.	**Mhe. Salama Aboud Talib**	**-**	**MBM/Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati / Nafasi za Wanawake**
19.	**Mhe. Sira Ubwa Mamboya**	**-**	**MBM/ Waziri wa Ujenzi,**

			Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
20.	**Mhe. Juma Ali Khatib**	**-**	**MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Uteuzi wa Rais**
21.	**Mhe. Said Soud Said**	**-**	**MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Uteuzi wa Rais**
22.	**Mhe. Khamis Juma Mwalim**	**-**	**Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe**
23.	**Mhe. Mihayo Juma N'hunga**	**-**	**Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais /Jimbo la Mwera**
24.	**Mhe. Shamata Shaame Khamis**	**-**	**Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Micheweni**
25.	**Mhe. Harusi Said Suleiman**	**-**	**Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete**
26.	**Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri**	**-**	**Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani**
27.	**Mhe. Mohamed Ahmada Salum**	**-**	**Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/Jimbo la Malindi**
28.	**Mhe. Chum Kombo Khamis**	**-**	**Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale/ Nafasi za Wanawake**

29.	**Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Uwezeshaji,**	**-**	**Naibu Waziri wa Wazee, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake**
30.	**Mhe. Lulu Msham Abdalla**	**-**	**Naibu Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo/ Nafasi za Wanawake**
31.	**Mhe. Juma Makungu Juma**	**-**	**Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba , Maji na Nishati / Jimbo la Kijini**
32.	**Mhe. Hassan Khamis Hafidh**	**-**	**Naibu Waziri wa Biashara, na Viwanda /Jimbo la Welezo**
33.	**Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi**	**-**	**Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Mtopepo**
34.	**Mhe. Abdalla Ali Kombo**	**-**	**Jimbo la Mwanakwerekwe**
35.	**Mhe. Ali Khamis Bakar**	**-**	**Jimbo la Tumbe**
36.	**Mhe. Ali Salum Haji**	**-**	**Jimbo la Kwahani**
37.	**Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)**	**-**	**Jimbo la Kijitoupele**
38.	**Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil**	**-**	**Uteuzi wa Rais**
39.	**Mhe. Ame Haji Ali**	**-**	**Jimbo la Nungwi**
40.	**Mhe. Amina Iddi Mabrouk**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
41.	**Mhe. Asha Abdalla Mussa**	**-**	**Jimbo la Kiwengwa**
42.	**Mhe. Bahati Khamis Kombo**	**-**	**Jimbo la Chambani**
43.	**Mhe. Bihindi Hamad Khamis**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
44.	**Mhe. Hamad Abdalla Rashid**	**-**	**Jimbo la Wawi**
45.	**Mhe. Hamida Abdalla Issa**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
46.	**Mhe. Hamza Hassan Juma**	**-**	**Jimbo la Shaurimoyo**
47.	**Mhe. Hidaya Ali Makame**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
48.	**Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)**	**-**	**Jimbo la Mtoni**

49.	**Mhe.**	**Jaku Hashim Ayoub**	**-**	**Jimbo la Paje**
50.	**Mhe.**	**Khadija Omar Kibano**	**-**	**Jimbo la Mtambwe**
51.	**Mhe.**	**Machano Othman Said**	**-**	**Jimbo la Mfenesini**
52.	**Mhe.**	**Makame Said Juma**	**-**	**Jimbo la Kojani**
53.	**Mhe.**	**Maryam Thani Juma**	**-**	**Jimbo la Gando**
54.	**Mhe.**	**Masoud Abrahman Masoud**	**-**	**Jimbo la Bububu**
55.	**Mhe.**	**Miraji Khamis Mussa**	**-**	**Jimbo la Chumbuni**
56.	**Mhe.**	**Moh'd Mgaza Jecha**	**-**	**Jimbo la Mtambile**
57.	**Mhe.**	**Mohamed Said Mohamed**	**-**	**Jimbo la Mpendae**
58.	**Mhe.**	**Mohammedraza Hassanaali Mohamedali**	**-**	**Jimbo la Uzini**
59.	**Mhe.**	**Mtumwa Peya Yussuf**	**-**	**Jimbo la Bumbwini**
60.	**Mhe.**	**Mtumwa Suleiman Makame**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
61.	**Mhe.**	**Mussa Ali Mussa**	**-**	**Jimbo la Ole**
62.	**Mhe.**	**Mussa Foum Mussa**	**-**	**Jimbo la Kiwani**
63.	**Mhe.**	**Mwanaidi Kassim Mussa**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
64.	**Mhe.**	**Mwantatu Mbaraka Khamis**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
65.	**Mhe.**	**Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini**	**-**	**Jimbo la Dimani**
66.	**Mhe.**	**Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy**	**-**	**Jimbo la Chaani**
67.	**Mhe.**	**Nassor Salim Ali**	**-**	**Jimbo la Kikwajuni**
68.	**Mhe.**	**Omar Seif Abeid**	**-**	**Jimbo la Konde**
69.	**Mhe.**	**Panya Ali Abdalla**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
70.	**Mhe.**	**Rashid Makame Shamsi**	**-**	**Jimbo la Magomeni**
71.	**Mhe.**	**Saada Ramadhan Mwendwa**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
72.	**Mhe.**	**Said Omar Said**	**-**	**Jimbo la Wingwi**
73.	**Mhe.**	**Said Hassan Said**	**-**	**Mwanasheria Mkuu**
74.	**Mhe.**	**Salha Mohamed Mwinjuma**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
75.	**Mhe.**	**Salma Mussa Bilal**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
76.	**Mhe.**	**Shaib Said Ali**	**-**	**Jimbo la Chonga**
77.	**Mhe.**	**Simai Mohammed Said**	**-**	**Jimbo la Tunguu**
78.	**Mhe.**	**Suleiman Makame Ali**	**-**	**Jimbo la Ziwani**
79.	**Mhe.**	**Suleiman Sarahan Said**	**-**	**Jimbo la Chakechake**
80.	**Mhe.**	**Tatu Mohamed Ussi**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
81.	**Mhe.**	**Ussi Yahya Haji**	**-**	**Jimbo la Mkwajuni**
82.	**Mhe.**	**Viwe Khamis Abdalla**	**-**	**Nafasi za Wanawake**

83.	**Mhe.**	**Wanu Hafidh Ameir**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
84.	**Mhe.**	**Yussuf Hassan Iddi**	**-**	**Jimbo la Fuoni**
85.	**Mhe.**	**Zaina Abdalla Salum**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
86.	**Mhe.**	**Zulfa Mmaka Omar**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
	Ndg.	**Raya Issa Msellem**	**-**	**Katibu**

Kikao cha Thelathini na Tatu– Tarehe 29 Juni, 2018

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Zubeir Ali Maulid) alisoma dua

TAARIFA YA SPIKA

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, Katika Kikao cha Baraza cha tarehe 25 Juni, 2018, Mheshimiwa Rashid Makame Shamsi aliuliza swali la nyongeza lililotokana na swali la msingi namba 225. Mheshimiwa Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo aliahidi kujibu kwa maandishi.

Sasa namuomba Mheshimiwa Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo asome jibu la swali la nyongeza lililoulizwa na Mjumbe huyo. Mhe. Waziri karibu sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mheshimiwa Rashid Makame Shamsi Mwakilishi swali lake ambalo nilimuahidi nitamjibu kwa maandishi kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2017/2018 jumla ya wasanii 14 walitembelewa na Wizara yangu kwa lengo la kuwafariji na kuwapa moyo juu ya changamoto wanazokabiliana nazo na kuangalia hatua za kufaa katika kuwasaidia. Napenda kiliarifu Baraza lako Tukufu kwamba pia kazi hii ilifanywa na Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii ya Baraza la Wawakilishi ambapo waliwatembelea wasanii wanne (4) wakiwemo Fatma Issa, Mohamed Ilyassi, Bi Mariam Hamdani na Bi Mwanacha Hassan. Lengo ni kuwafariji wasanii hawa na kuwapa moyo juu ya maisha yao lakini pia kujua changamoto zinazowakabili hatimaye kuishauri Wizara yangu juu ya kuangalia hatua za kufaa katika kuwasaidia.

(b) Mhe. Spika, Katika kukabiliana na hali hii jitihada mbali mbali zimeendelea kuchukuliwa na Wizara katika kuhakikisha maslahi ya Wasanii wetu yanalindwa kwa mujibu wa sheria. Wizara kupitia Taasisi ya Haki Miliki inawajibu wa kusimamia kazi za wasanii wetu na kusimamia haki zao kisheria kwa wasanii wote. Jumla ya wasanii 14 kutoka Pemba na 20 kutoka Unguja wamefuatwa kwenye makaazi yao na kukabidhiwa mirabaha yao iliyotokana na kazi zao za ubunifu na sanaa yenye jumla ya shilingi 3,400,000/-

Hata hivyo, Wizara haikusita kuchukua hatua za kuwasaidia wasanii hawa kila ilipowezekana katika kufanikisha shughuli zao. Kwa mfano msanii Fatma Issa ambaye ni mtunzi na muimbaji wa nyimbo za taraabu alisaidiwa shilingi 490,000/- katika kuzalisha CD zake ili aendelee na mauzo ya kazi zake. Ahsante sana Mhe. Spika.

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha Mezani Mswada wa Sheria ya Kuweka Masharti Bora ya Usimamizi wa Mahakama, Kufafanua Utumishi wa Mahakama, Kuanzisha Ofisi za Mtendaji Mkuu wa Mahakama na Mrajis, Kuanzisha Mfuko wa Mahakama na Kuweka Masharti Mengine Yanayohusiana na Hayo.

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha Mezani Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu na Kuweka Masharti ya Ukaguzi wa Elimu pamoja na Mambo Mengine Yanayohusaiana na Hayo. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais (Kny. Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha Mezani Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Wakala wa Serikali ya Uchapaji Zanzibar na kuweka masharti bora yanayohusiana na Kazi, Uwezo, Uongozi na Mambo mengine Yanayohusiana na Hayo. Naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 106

Kutotambuliwa kwa Pasi za Wanafunzi

Mhe. Jaku Hashim Ayoub (Kny. Mhe. Hidaya Ali Makame) – Aliuliza:

Hivi karibuni kumetokea mkanganyiko kwa baadhi ya wanafunzi wanaotoka kidato cha nne kwenda Kidato cha Sita ambao wamepata matokeo yao ya mtihani wa Taifa 2017/2018 na kuonekana kuwa wamepasi, hata hivyo baadhi ya wanafunzi hao ambao matokeo yanaonesha wamepasi Wizara haitambuwi pasi hizo na badala yake wamekosa nafasi za kujiunga kidato cha sita.

(a) Wizara inaweza kueleza utaratibu wa pasi na kombi za kujiunga Kidato cha Sita.

(b) Je, ni kwa kiasi gani vijana hao ambao pasi zao hazitambuliwi hawajakidhi vigezo hivyo.

(b) Wizara inawasaidia vipi vijana ili waweze kuendelea na masomo endapo itaonekana kuna makoseo yamefanyika kwa kuzikataa pasi zao.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:

Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Hidaya Ali Makame swali lake Nam. 106 lenye vifungu (a), (b) na (c) kwanza naomba kutoa maelezo kama ifuatavyo:-

Wizara ya Elimu na Mafunzo Amali inadahili wanafunzi waliohitimu Kidato cha Nne ambao wamepata sifa za kujiunga na Kidato cha Tano. Utaratibu unaotumika katika kudahili ni sawa na unaotumika Tanzania Bara ambao wanafunzi wote wanatakiwa watimize sifa za kufanya Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Sita unaoandaliwa na Baraza la Mtihani la Tanzania (NECTA).

Baada ya maelezo naomba kumjibu kama ifuatavyo:-

(a) Wanafunzi wanaojiunga na Kidato cha Tano wanatakiwa wawe na sifa zifuatazo:-

i. Ufaulu wa angalau *Credit* tatu na D mbili za masomo.

ii. Kwa mwanafunzi anaefanya mtihani kama ni mtahiniwa wa skuli asizidi umri wa miaka 24 wakati atakapofanya Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Sita.

iii. Awe na masomo ya tahasusi (masomo yanayolingana) na wengine wanayatambua kama *combination* zinazotambulika na kufanyiwa mitihani.

Uchambuzi wa masomo ya tahasusi ni kama hivi ifuatavyo:-

- Tahasusi za Sayansi ambazo ziko 4 nazo ni: PCM, PCB, BCG, na PGM
- Sanaa ziko 10: AKL, HKL, HGL, HGK, KAR, AHG, AHK, KLF, HLF na KLG.
- Biashara kuna 3: ECA, EGM, PCOM.

Wanafunzi wanaochaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano ni lazima watimize sifa hizo.

(b) Wanafunzi wasiotimiza sifa hizo wanashauriwa kujiendeleza kwa kusoma tena na kufanya mtihani kama watahiniwa wa faragha.Wanafunzi wengine wasio na sifa za kujiunga na masomo ya Kidato chaTano na wanatimiza sifa za kujiunga na vyuo vyengine, wanachaguliwa kujiunga na mafunzo ya ualimu ngazi ya Cheti au Diploma au katikaVituo vya Mafunzo ya Amali.

(c) Wanafunzi wasiotimiza sifa za kujiunga na vyuo hushauriwa kujiendeleza na kurudia mtihani ili waweze kutimiza sifa za kujiunga na taasisi nyengine za elimu ikiwemo kozi za ukutubi, usekretari na huduma mbali mbali za afya na mafunzo ya ufundi katika Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia. Ahsante sana.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ninavyoingalia karatasi lilivyoulizwa swali na Mhe. Hidaya Ali Makame hivi karibuni kumetokea mkakanganyiko wa baadhi ya wanafunzi wanaotoka Kidato cha Nne kwenda kidato cha Sita ambao wamepata matokeo ya mtihani wa Taifa na kuonekana kuwa wamepasi.

(a) Mhe. Spika, nilikuwa nataka kujuwa hili swali alilouliza ni kweli kumetokea mkakanganyiko huo na kama haukutokea utueleze na kama umetokea mmechukuwa hatuwa gani ndio swali la msingi alilouliza Mhe. Hidaya Ali Makame.

(b) Ili mwanafunzi afanye vizuri inategemea na mazingira yawe mazuri kufaulu kwake ni sababu gani zilizopelekea hata Skuli yangu kushika mkia Jimbo la Paje Mtule, kutokana na mazingira ya Skuli ile pengine Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali nayo imechangia kuvuja kwa muda mrefu na hamujachukua hatua yoyote mpaka muda huu, lini mtachukua hatua hiyo kwenda kushughulikia skuli ile na kwa faida ya Baraza hili

hebu tueleze hii AKL, HKL, HGL, HGK, KAR, AHG, KHL, KLF, HLF, KLG na ECA, EGM, PCoM kwa faida ya baraza hili na kwa ajili ya wananchi nini maana yake kwa urefu.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yakoa naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub maswali yake ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, kuhusu mkanganyiko kulikuwa na mazowea kwamba mwanafunzi yoyote wa Kidato cha Nne akipata *credit* 3 anaweza kuchaguliwa kusoma masomo ya kidato cha Tano ambapo fursa hiyo itakuwepo lakini kuna marekebisho yamefanyika na wala sio marekebisho lakini utekelezaji umefanyika kwamba si *creditii 3* peke yake lakini angalau awe na D 2 kwa pamoja hizi 3 na 2 ziweze kuunda masomo ya siyopungua matano hayo ndiyo yanayotambulika ni masomo ya kuweza kuendelea na masomo ya juu tafauti na zamani kidogo ilikuwa *credit* 3 ukiweza kusoma kwa hivyo hayo ndio jambo lililowachanganya wanafunzi na bila ya shaka Wizara imetowa ufafanuzi na wote ambao wana sifa tumeweza kuwadahili na kuwachukua katika Kidato cha Tano kwa taarifa yenu tu mwaka huu tumechukua wanafunzi 2,564 kujiunga na Kidato cha Tano.

(b) Mhe. Spika, na kuhusu lini Paje – Mtule itatengenezwa hii kwa kweli tunasubiri kwa sasa maoni ya Kamati Teule baada ya hapo tunaweza kuuamua vipi ifanyike.

Mhe. Spika, na kuhusu ufafanuzi wa hizi tahasusi ningechukuwa fursa hii kufafanua kama ifuatavyo:--

AKL maana yake ni Arabic, Kiswahili na Language na language maana yake hapa kiingereza

HKL maana yake ni History, Kiswahili Language

HGL maana yake ni History, Geography Language

HGK maana yake ni History Geography Kiswahili

KAR maana yake ni Kiarabu, Arabic na Religion

AHG maana yake ni Arabic, History na Geograhpy

AHK maana yake ni Arabic, History na Kiswahili

KLA maana yake ni Kiswahili, Language and French

HLF maana yake ni History, Language and French

KLG maana yake ni Kiswahili, Language and Geography

Nam. 185

Bei Ndogo ya Zao la Mwani

Mhe. Suleiman Sarahan Said (Kny. Mhe. Asha Abdalla Mussa) – Aliuliza:

Kwa muda mrefu wakulima wa mwani wamekuwa wakilalamikia bei ndogo ya zao hilo kulinganisha na kazi kubwa wanayoifanya katika kilimo hicho.

Je, Wizara kwa mwaka wa fedha 2018/2019 imejipanga vipi kuhakikisha kuwa zao hilo linapanda bei na kuwafanya wakulima kufaidika na kilimo hicho.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi - Alijibu:

Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii ya kujibu swali Nam. 185 kwanza kabisa kabla sijajibu swali hili naomba nitoe maelezo kuhusu zao la mwani naita maelezo haya ni miujiza ya mwani.

Mhe. Spika, mwani ni zao muhimu sana la kiuchumi ambalo linawashirikisha wananchi wasiopungua elfu 23,654 linasaidia sana kupata kipato 80% ya hao ni wanawake na nikisema Zanzibar ni nchi ya tatu kuzalisha mwani duniani ingawa mwani wake bado ni kidogo ni karibu 5% tu ya mahitaji ya mwani wa dunia. Mwani una matumizi mengi sana yakiwemo chakula, na ni chanzo kikuu cha *vitamin* A, B, C, D, E na K na Madini ikiwemo Iodine, Calcium, Potation, Magnesium, manganese na kadhalika hutumika kama mbolea, hutumika kwa kutengenezea bidhaa za viwandani, vipodozi, manukato, rangi, waya za kuchomea chuma na kadhalika hutengenezewa pia dawa za binadamu.

Sasa Mhe. Spika, kwa ruhusa yako sasa naomba kumjibu Mhe. Asha Abdalla Mussa swali lake Nam. 185 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Wizara kwa mwaka wa fedha 2018/2019 imejipanga kuendesha mafunzo ya usarifu na kuongeza thamani zao la mwani ili kupata bidhaa ambazo zitatumika katika soko la ndani na hivyo kupunguza utegemezi wa soko la nje ya nchi peke yake ambalo hivi sasa bei yake ni ndogo. Ushiriki wa wajasiriamali wa mazao ya mwani katika maonyesho mbali mbali nchini yatasaidia kutangaza bidhaa hizo zinazotokana na mwani.

Aidha, kwa mashirikiano na Wizara ya Biashara, na washirika wa maendeleo na wadau wa mwani yanaendelea ili kuhakikisha kuwa zao la mwani linapanda bei na kuwafanya wakulima kufaidika na kilimo hicho. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nakushukuru sana Mhe. Spika, na mimi na ni mshukuru Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa majibu yake mazuri lakini tatizo kubwa ambalo tunalilalamikia sana ni bei ya wakulima kutokana na kazi zake ni kama kitu cha karafuu kwamba kina kazi nyingi, kuvuna, kuanika, kufanya kitu gani. Sasa na hivi karibuni Mhe. Waziri alisema huwenda tukawa na kiwanda hapa ambacho kinaweza kikazalisha baadhi ya bidhaa kutokana na mwani sasa Mhe.

Nimuulize tu kwamba katika mtitiriko wa maeneo ambayo sasa hivi yanalimwa mwaji Je kwa upande wa Zanzibar lakini nasema Unguja na Pemba yote je kuna mpango wa kilimo hichi baada ya maeneo haya kwamba ni maeneo yaliyotengwa na maeneo mengine ambayo uzalishaji wake na kwa aina nyengine ambayo wenzetu kama kutoka huku nchi ambazo wanalima mwani ziko kabila zake, maana yake nazungumzia kabila hapa kwamba kuna kabila za mwani ambazo labda zina *rank* nzuri kutokana na mambo yake. Hapa Zanzibar tumeshapata mbegu hizo ambazo zina *high quality*.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Suleiman Sarahan Said swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwa kushirikiana na Wizara ya Biashara na Wizara nyengine zote zitakazohusika upo mpango mahususi wa kuwa na kiwanda cha kusarifu mwani ambacho kwa kweli kitatoa bidhaa mbali mbali ambazo pia zitaweza kuongeza thamani ya bei ya mwani kwa kilo, badala ya ile iliopo sasa hivi ya Sh. Miaka 5. Kwa hivyo napenda kumuahidi Mhe. Mjumbe kwamba asiwe na wasiwasi suala lake hilo ni zuri sana na sisi tunalifanyia kazi na ni lengo letu kabisa kabisa kuwa na kila kitu kinachostahiki kuwepo hapa kwa ajili ya kusarifu mwani ili mapato ya wananchi yaweze kupatikana na zile bidhaa zote zinazoweza kutokana na mwani ikiwa madawa, mbolea pia tuweze kuzalisha hapa hapa nchini. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na mipango mzuri ya wizara na kutokana na malalamiko makubwa yanayotokana na wakulima wa zao hili la mwani kuhusu bei yake. Je, ni hatua gani pamoja na mikakati ambayo wizara imechukua ili kuona zao hilo linaongezewa bei kwa lengo la kuwatia moyo wakulima wa zao hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Kuna njia mbali mbali za kuongeza bei ya mwani au kipato cha mwani. Kwanza unaweza ukaongeza kipato cha mwani kwa kulima eneo kubwa zaidi. Pili, unaweza ukaongeza kwa hivyo tulivyosema kwamba unaongeza thamani, unatoa bidhaa mbali mbali kutokana na mwani kama vile *jam*, vipodozi na mambo mengine. Hayo pia yatasaidia kuongeza thamani ya mwani. Kwa hivyo, tusiwe na wasiwasi wajumbe bei ya mwani itapanda *automatically*.

Mhe. Spika, lakini kuna tatizo moja kama tunategemea nje kwa bei iliyoko nje mwani utaendelea kuwa na bei hii, kwa sababu huko nje bei ya mwani sio kubwa kama vile tunavyotegemea. Kwa sababu hapa tunanunua karibu shilingi 500 kule labda dola moja na nusu mpaka mbili au tatu. Sasa ukisafirisha mpaka kupeleka kule inakuwa hawapati faida kubwa kwa hivyo, wanaamua waweke bei hiyo. Lakini hata hivyo, tutakapokuwa na hivyo viwanda vya kusarifu bei ya mwani itapanda. Pia wakulima nawaomba wasivunjike moyo kuhusu bei kwa sababu mwani ulianza shilingi 1,940 hapa, watu walianza kuokota mwani walikuwa hawapandi, lakini walikuwa wanauokota unauzwa chini ya shilingi mbili kwa kilo. Mwaka 1998 ulipoanza mwani rasmi bei ikapanda ikawa

shilingi 20, imekwenda shilingi 200, shilingi 300 mpaka leo shilingi 500. Kwa hivyo, tunategemea sana na huko mbele bei itapanda wakulima wasivunjike moyo mwani umewasaidia sana. Kuna wengine wamejenga nyumba, wengine wamesomesha watoto wao skuli na kadhalika. Kwa hivyo, tusivunjike moyo bei ya mwani itapanda pole pole kadiri tunavyokwenda. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kidogo sauti zenu zinasumbua kule kwenye *hansard* taarifa niliyonayo na baada ya hapo nimekuona Mhe. Jaku Hashim Ayoub kwa swali la nyongeza.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, Mhe. Naibu Waziri katika majibu yake amesema wizara kwa mwaka wa fedha 2018/2019 imejipanga kuendesha mafunzo hayo. Hebu Mheshimiwa anaweza kutwambia wamejipanga kutoka wapi mpaka wapi na hii foleni imeanzia wapi mpaka wapi. Hiki kilio kimekuwa cha muda mrefu na agizo la Mhe. Rais aliagiza wizara nne, ikiwa Wizara ya Afya, Wizara ya Biashara na Viwanda, Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, wamejipanga kutoka wapi mpaka wapi ili wananchi wapate kufahamu hasa wa Jimbo la Paje maana wamepata neema ya kuzungukwa na bahari atueleze hii foleni itamalizika lini kutatua tatizo hili.

La pili, kuna ahadi ya vihori 500 kutolewa anaweza kutwambia sehemu gani vimefika vihori hivi kwa ajili ya kuwasaidia wananchi au wakulima hao wa mwani.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Spika, namshukuru Mhe. Jaku Hashim Ayoub kwa swali lake zuri sana na kutaka kujua tulivyojipanga. Napenda kumthibitishia Mhe. Mjumbe tumejipanga kweli kweli kuongeza mapato ya mwani, kuendeleza zao la mwani. Naweza kusema kwamba kama nilivyosema kabla kuwa tunakusudia kutoa bidhaa tafauti kutokana na zao la mwani. Zao la mwani nilisema hapo mwanzo kwamba linatumika kutengeneza kachumbari, chakula, mambo ya vipodozi na mambo mengine. Hayo ndio tutakayokuwa tunayasisitiza yafanyike hapa nchini na pia tutaongeza *average*. Napenda kumwambia kwamba kuna vijiji 80 hapa Unguja vinalima mwani na vingi vyao tumeshavitembelea, tumeshaona, tumeshasikia matatizo yao. Kwa hivyo, kila tatizo linalosababisha mwani usiendelee vizuri basi tutalitatua na miongoni mwa matatizo hayo ambayo tunataka kuyatatua sasa hivi ni matatizo ya magonjwa ya mwani ambayo pia yanasababisha kupungua bei.

Utaratibu

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Swali langu la pili hakulijibu kuhusu vihori 500.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri anazungumza.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Spika, kama ilivyo kawaida niendelee kumpongeza Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa kutoa majibu ambayo ni sahihi na yenye takwimu kamili kutokana na zao hili la mwani.

Mhe. Spika, ni kweli kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri tumejipanga na tumejipanga kipindi kirefu. Sisi sote hapa mashahidi mwaka jana tumeona namna gani mwani tunavyoweza kuusarifu kuleta mazao mengine. Ndani ya Baraza lako tukufu tumeshaonesha jinsi mwani unavyoweza kutumika ukawa sabuni, mwani unavyofanyiwa keki, unavyofanyiwa mazao mengine tafauti ambayo yanatokana na mwani.

Suala la kuweza kuwazidishia bei wananchi ni suala muhimu wananchi wengi wanalima mwani, wananchi wengi wana matumaini. Kazi yetu Wizara ya Kilimo kuendelea kuwahamasisha na kuwashajihisha wananchi waendelee kulima zao hili ili waweze kuendeleza ajira zao kuweza kuiongezea serikali mapato na kuinua uchumi wa nchi hii.

Mhe. Spika, lakini katika hilo napenda niwaambie wananchi kwamba ili kuliongezea bei zao letu la mwani ni kama lilivyo zao la karafuu, kinachotakiwa sasa hivi kuelekea kwenye mfumo kamili wa biashara katika ukulima huu tunaoulima. Yaani kwa kushirikiana na Wizara ya Biashara na Viwanda tunaendeleza zao la mwani kulifanyia *branding* na *package* ili liweze kukubalika kimataifa na ndani ya soko letu. Kwa hivyo, kwa mfumo wa kulifanyia *package*, mfumo wa kuweza kuli-*distribute* kwa njia ya *branding* nina hakika zao la mwani litapanda bei na wananchi wetu wataweza kunufaika na bei. Nakushukuru sana Mhe. Spika. *(Makofi)*

Nam. 87

Ujenzi wa Daraja la Kitope

(Mhe. Mjumbe aliyetaka kuuliza swali hili ameliondoa)

Nam. 249

Maegesho Maalum ya Magari ya Uokozi

Mhe. Ali Khamis Bakar – Aliuliza:

Naipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kununua magari ya Uokozi katika Kiwanja cha Ndege cha Abeid Amani Karume ili kutoa huduma bora na kwa kuwa magari haya yamenunuliwa kwa gharama kubwa na yanahifadhiwa bila ya kuwekwa katika maegesho maalum hali inayosababisha magari hayo kuharibika.

(a) Je, ni lini yatajengewa sehemu ya maegesho ili yasipigwe na jua na mvua.

(b) Ni kiasi gani cha fedha kinachohitajika katika ujenzi wa banda hilo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais (Kny. Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 249 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, Magari ya Uokozi katika Kiwanja cha Ndege cha Abeid Amani Karume yapo ili kutoa huduma bora na magari haya yamenunuliwa kwa gharama kubwa na yanahitaji hifadhi ya kuwekwa katika maegesho maalumu. Hali hii ya magari hayo ili magari hayo yasiharibike.

Mamlaka ya Viwanja vya Ndege imejenga banda la kuhifadhia Magari ya Zimamoto pamoja na ofisi za kutoa huduma upande wa kusini wa kiwanja ambapo magari hayo yanahifadhiwa, lakini hayatoshi kuyaweka magari yote manne. Mamlaka pia ilijenga banda la ziada karibu na kituo cha zamani cha Zimamoto kwa ajili ya kusaidia kuhifadhi gari zitazokuwepo eneo hilo. Hata hivyo, banda hilo halikukidhi haja kutokana na urefu na upana wa magari hayo.

Mamlaka imeliona tatizo hilo na tayari imeshaanza hatua za kutayarisha ujenzi wa banda jengine katika kituo hicho kwa ajili ya kuhifadhi gari zinazotoa huduma katika eneo hilo la Uwanja wa Ndege.

(b) Mhe. Spika, makisio ya ujenzi wa banda hilo ni TZ.Shs 10,000,000/=.

Mhe. Ali Khamis Bakar: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako kwanza nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini vile vile niipongeze wizara kwa kuliona hilo na wakaweza kujenga haya mabanda likiwemo la kwanza, la pili na sasa hivi ikiendelea na ujenzi wa banda la tatu. Lakini naomba niulize swali la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Waziri ujenzi wa banda la mwanzo na hili la pili ni kiasi gani cha gharama kiligharimu, lakini na hili la pili ambalo linaendelea na ambalo limewekewa makisio hapa shilingi 10,000,000. Je, ni lini litamalizika. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo. Kwenye swali lake la mwanzo alilotaka kujua gharama za mabanda haya Mheshimiwa kwa sababu ni jambo linahitaji takwimu kwa sasa sina takwimu hizo. Kwa hivyo, naomba kulihakikishia Baraza lako tukufu nitawasiliana na wizara husika ili apate idadi kamili ya gharama za ujenzi wa banda la kwanza na la pili.

Hata hivyo, banda hili jengine linalojengwa halitochukua muda mrefu litakuwa tayari kwa ajili ya matumizi. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Machano Othman Said: Ahsante Mhe. Spika. Kwanza naomba nimshukuru Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kwa majibu yake ya ufasaha. Lakini pamoja na majibu hayo naomba niulize swali la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwa muda mrefu kumekuwa na mgogoro wa uendeshaji katika taasisi ya Uwanja wa Ndege na Zimamoto kuhusu uwekaji wa maji katika hodhi la airport kile kituo kipya cha Zimamoto kwamba hakuna umeme na maji hamna kwa hivyo inakuwa shida katika

uokozi wa ndege zetu ikitokea ajali. Lakini pia *assess road* kule kutoka kwenye kituo mpaka kwenye uwanja nayo ni mbovu na inahitaji matengenezo.

Je, ni lini serikali itamalizia shughuli hizo ili huduma za *airport* ziwe katika hali bora na kutoa huduma kwa wananchi na ndege za kimataifa.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza. Ni kweli kulikuwa na matatizo hayo aliyoyasema Mhe. Mwakilishi lakini kwa sasa wizara na watu wa Zimamoto wamelishughulikia ipasavyo tatizo hilo. Nataka nimhakikishie Mhe. Mjumbe kuwa muda si mrefu matatizo haya yataondoka kabisa katika kiwanja chetu cha ndege ili uwanja wetu wa ndege utoe huduma bora kwa wananchi wote. Ahsante sana.

Nam. 25

Kupatiwa Zawadi Wakulima na Wauzaji Bora wa Karafuu

Mhe. Mussa Foum Mussa - Aliuliza:-

Wizara ya Biashara na Viwanda kupitia Shirika lake la *ZSTC* katika matarajio yake ya mwaka 2017/2018 ni kuwapatia zawadi wakulima na wauzaji bora wa karafuu.

(a) Je, waziri ahadi hiyo anaifahamu.

(b) Je, amechukua hatua gani ya kuitekeleza.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 25 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Shirika la Biashara la Taifa limekuwa likitoa zawadi ya pesa taslim kwa wakulima kila mwaka kuanzia mwaka 2014/2015, utaratibu ambao unaendelea kila mwaka ikiwemo mwaka 2017/2018.

(b) Utekelezaji wa utoaji wa zawadi hizo unafanyika kwa kila mwaka na kwa mwaka huu wa 2017/2018 Shirika limetenga kiasi ya TZS. 24,000,000.00 na tayari matayarisho yote ya utoaji wa zawadi hizo na vyeti maalum yamekamilika na tayari zimeshatolewa Mwezi wa Mei, 2018 wakati wa mikutano ya wakulima na wadau wa zao la karafuu. Ahsante.

Mhe. Mussa Foum Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba niulize swali moja la nyongeza. Kwanza naipongeza serikali kwa kuwa na utaratibu wa kutoa zawadi kwa wakulima wa zao la karafuu.

Mhe. Spika, kwa mara hii ni wauzaji wangapi bora waliopata zawadi hiyo ya pesa na ni kiasi gani kwa kila mmoja pesa alizozipata.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Mheshimiwa kwanza utaraibu huu ni utaratibu ambao Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia *ZSTC* umeuweka katika kuwa-*emphasize* wakulima kuendelea kulilima zao bora la karafuu kwa maslahi ya nchi yetu.

Mhe. Spika, tuna utaratibu tunakuwa tunatoa kila wilaya kwa maana hiyo wilaya nne za Pemba watu wamefaidika na wilaya tatu za Unguja. Kiasi ya watu waliofaidika wakulima na wauzaji bora wa karafuu ni watu 16 na idadi waliyopata kila mtu takribani shilingi 1,500,000/-. Ahsante.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nakushukuru sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii nami nimshukuru waziri kwa majibu yake mazuri. Lakini nataka nimwambie kwamba katika uchumaji wa karafuu kuna masuala ya kukodi na kuna masuala ya mwenye shamba, kigezo kinachotumika kumpata mtu huyu ambaye anakuwa kwa upande wa shirika anapewa zawadi ni mwenye shamba au ni utaratibu gani unaotumika kupatikana kwa mtu huyo ambaye anapewa zawadi. Kwa sababu nazungumza kwenye karafuu kuna kukodi na mwenye shamba. Sasa nyinyi utaratibu gani mnaotumia kumpa zawadi huyu mtu.

Suala la pili amesema kwamba *amount* ya mara hii ni shilingi 24,000,000/- ndio iliyotengwa kufanywa zawadi, anatumia kigezo gani ni *percentage* katika utafutaji wake wa mapato au inakuwaje katika shilingi 24,000,000/-.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Mheshimiwa utaratibu ambao *ZSTC* tumejiwekea ni kumpa mkulima bora na muuzaji bora wa zao la karafuu. Kadhalika pesa tulizozitenga baada ya kujadiliana kama taasisi huwa tunasema kasma hii irudi kwa wauzaji bora na wakulima. Kwa mwaka huu wa fedha 2017/2018 tulitenga shilingi 24,000,000 ambazo tuliwapa wakulima bora na wauzaji bora wa zao la karafuu.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri amesema kwamba wanatoa ahadi za kuwapa zawadi, Mhe. Waziri katika ahadi ni vizuri mtu kukamilisha ahadi. Mhe. Waziri wa Biashara na Viwanda mama yangu hapo Mhe. Amina Salum Ali aliwataka masheha wa kisiwani Pemba kudhibiti magendo ya karafuu kuhakikisha kwamba karafuu zinauzwa *ZSTC* ili serikali kupata mapato. Masheha wale aliwaahidi kwamba watapatiwa vespa kwa mikopo kukatwa ile mishahara yao, hadi leo hii masheha wale wanalalamika na wanatupigia simu wanataka kuuliza. Je, ahadi hii imekuwaje mpaka leo ni lini masheha wale watapatiwa vespa ili waweze kuwa na moyo zaidi wa kuhakikisha kwamba wanazidhibiti karafuu zinauzwa *ZSTC* na serikali inapata mapato yake. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Biashara na Viwanda: Mhe. Spika, naomba nijibu suala la nyongeza la Mhe. Suleiman Makame Ali kuhusu utaratibu wa vespa.

Ni kweli Mhe. Spika, mwaka jana kwa sababu karafuu zilikuwa ni nyingi na matishio ya kufanyiwa magendo pia yalikuwa makubwa lakini pia kwa kuwapa motisha wale wote ambao wanashughulikia na suala la karafuu kwa utaratibu wa kudumi tuliwaahidi kweli Masheha kwamba tutawapatia vespa na utaratibu huo tunaukamilisha na tulisema nadhani nimeomba nimuweke sawa Mhe. Suleiman Makame Ali kwamba tutawapatia fedha hizo kabla ya msimu unaokuja, na msimu unaokuja bado hatuanza. Kwa hiyo, vespa zao zitakamilika na watapatiwa wakati tulivyokuwa tumeahidi.

Lakini Mhe. Spika,naomba vile vile nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa majawabu mazuri aliyokuwa ameyatoa kuhusu zawadi ambazo tunazitoa kwa wakulima. Zawadi zinatolewa kwa wakulima kuangalia yule mkulima ambaye anaweza kwenda kuuza karafuu *ZSTC* zilizokuwa za kwanza wa pili na wa tatu.

Kuna wale wanaopewa wilayani lakini vile vile kuna wale ambao tunawapa kitaifa wale ambao wanakuwa wanauza karafuu nyingi sana ndio ambao wanaopewa zawadi. Kama alivyojibu kwamba kuna milioni ishirini zimewekwa kwa ajili ya kazi hiyo wale wa wilayani walipewa milioni moja moja lakini bado wale wengine watakabidhiwa kitita chao kwa kazi nzuri ambayo wameifanya. Mhe. Spika, nashukuru. Ahsante.

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Ali Suleiman Ali nakupa upendeleo kwa umuhimu wake.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa upendeleo na mimi kuuliza swala dogo la nyongeza.

Mhe. Spika, kwanza niipongeze wizara kwa kushughulikia zao hili kubwa la karafuu na tunaamini kwamba karibu miaka ishirini naa iliyopita mwaka huu ulikuwa kama uliofatia kwa zao kubwa ambalo tumelipata katika nchi yetu.

(a) Kwa kuwa kuna motisha au uhamasishaji ili kila wilaya kila eneo watu wafanye vizuri katika kuvuna zao la karafuu na kutunza mikarafuu yetu. Katika Wilaya za Unguja na Pemba ni Wilaya gani iliofaidika na iliyofanya vizuri zaidi kuliko zote.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Biashara na Viwanda naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suala lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo:

Mhe. Spika, kama nilivyosema katika suala langu kwamba Wilaya zilizofaidika kwa Pemba ni Wilaya nne na Wilaya tatu kwa Unguja hizo ndizo Wilaya zilizofaidika.

Lakini Mhe. Spika, Wilaya ya Mkoani kama tunavyojua ndio wilaya inayolima karafuu nyingi kwa Zanzibar. Kwa maana hiyo na hiyo ndio wilaya iliyofaidika zaidi kwa sababu ndio inayolima karafuu nyingi kwa zao letu la karafuu Zanzibar. Ahsante Mhe. Spika.

Nam. 147

Matumizi ya Pampu zilizotolewa na Ras –El – Khaima

Mhe. Suleiman Sarahan Said (kny. Mhe. Simai Mohammed Said– Aliuliza**:**

(a) Je, ni pampu ngapi za maji zimetumika zilizotolewa na Ras El Khaima.

(b) Je, ni pampu ngapi zimebakia katika hizo na maeneo yaliotumika ndio yale yaliochimbwa visima na kampuni hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati – Alijibu**:**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe Mwakilishi swali Nam. 147 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

(a) Mhe. Spika, Pampu zilizotolewa na Ras–el- Khaimah kupitia Mradi wa uchimbaji wa visima uliofadhiliwa na mtawala wa Ras el Khaimah ni 150.

(b) Mhe. Spika, Pampu zote 150 zimeshatumika kwa kutiwa katika visima ambavyo pampu zake ziliharibika au kuungua kutokana na hitilafu mbali mbali hivyo ili kuhami hali hiyo na kutopata maji kwa wananchi pampu za Ras-El-Khaimah zilitumika wakati visima vilivyoungwa vikisubiri kuendelezwa, na baadhi ya pampu hizo zimetumika kwa visima vipya vilivyoendelezwa kupitia mradi huo. Ahsante sana.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Spika, nashukuru sana lakini pia nataka nimuulize kwamba pampu zilizoletwa kwa niaba ya Ras- el-Khaimah ni kwamba zilikusudiwa zaidi na kampuni hii kwa ajili ya vile visima vyao ambavyo walivitumia.

(a) Sasa Waziri haoni kwamba kwa mtizamo wa karibu kama pampu hizi alizikopa na anahitajika kuzirudisha.

(b) Lakini kwa mwaka huu wa 2018/19 amekusudia kununua pampu gapi ambazo zitakizi hizi pampu ambazo zilikopwa au nazungumzia kwamba zilikuwa za kampuni.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati: Ahsante Mhe. Spika, napenda kumjibu Mhe. Suleiman Sarahan Said suala lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

(a) Ni sahihi kusema kwamba kutumika kwa pampu zile ni sawa na kukopa kwa sababu tuna wajibu kama Mamlaka ya Maji *ZAWA* kuingiza pampu katika visima vile vilivyokuwa vimebakia na kazi hiyo tunaendelea.

(b) Kuhusiana pampu ngapi tumeagiza kwenye bajeti kama utaangalia vizuri tulisema tutaendeleza vile visima maalum takribani ishirini. Lakini ununuzi wa pampu

unaedelea maana hivi karibuni pia tumenunua pampu tunategemea na nguvu ambayo tutapata lakini na mahitaji ya visima husika si lazima kile ambacho kimetengezwa na Ras- el- Khaimah lakini pia tuna wajibu wa kuweka pampu katika kila kisima ambacho kinahitaji hivyo na ikiwa nguvu tunazo. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Ali Suleiman Ali : Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza.

Mhe. Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa kuona pana haja kwa kuwa baadhi ya visima mashine ziliungua zikawekwa zilizokuwepo ni sahihi ili wananchi wapate huduma.

(a) Kwa kuwa kuna baadhi ya visima ambavyo vipo mpaka havijawekewa mashine yoyote kutokana na ufinyu au kuwa hazipo na wizara iko mbioni katika kulitatua tatizo hilo. Hebu alieleza Baraza hili na wananchi wajue kila kisima cha Ras-el-Khaimah mashine yake inagharimu kiasi gani.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati: Ahsante Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Ali Suleiman Ali suala lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kikawaida pampu zinakuwa zinatafautiana kutokana na ukumbuwa kwa hivyo, kutokana na kisima husika ndipo tunajua hapa pampu gani inastahiki na hivyo bei yake tunaijua hapo. Ahsante sana.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Mimi nina suala dogo la nyongeza kama ifuatavyo:

Visima vya madi huu wa Ras- el- Khaimah vimechimbwa zaidi ya miaka nne sasa na bado hazijamalizwa kuwekwa vitendea kazi vyake. Hivi Mhe. Waziri anaweza kulieleza Baraza hili kisima ambacho hakijamalizika kinaweza kuchukuwa miaka mingapi kabla ya kuharibika tena na kuweza kutumika.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati: Ahsante Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Machano Othman Said suala lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza kabla ya kuchimba tunajitahidi sana kuona eneo gani ni zuri, zuri kwa maana ya mazingira yake lakini pia upatikanaji wa maji. Inapotokezea hali halisi au *natural* ya maumbile hii inakuwa ipo nje ya uwezo. Kwa hiyo, hatuna jawabu ya kusema kwamba inachukuwa muda fulani kwa maana kwamba tunapochimba kisima tunategemea kitoe huduma kwa kudumu.

Kwa hiyo, hatuna hesabu kwamba hapa tunachimba kisima kwa mwaka mmoja au miaka miwili kitakufa. Isipokuwa yale majaaliwa ya Mwenyezi Mungi yalitokezea yanakuwa

hatuna namna. Lakini kikawaida tunachimba katika maeneo ambayo visima hivyo tunategemea vidumu na vitoe huduma kwa jamii. Ahsante sana.

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, kwanza nikushukuru kwa kanuni ya 63 sijui utaniruhusu nisome au itakuwa imetosha baada ya 63 ije 45(27) kuhusu taarifa utaratibu.

Mjumbe anaweza kusimama wakati wowote na kusema neno kuhusu utaratibu lakini Mjumbe anapofanya hivyo itabidi atake kanuni ya Baraza la iliyokiukwa. Mjumbe yoyote ambaye wakati huu atakuwa anasema hapo hapo atakaa chini na kwa vile Mjumbe anaesimama kusema utaratibu atakaa chini na akeshaa kukaa jambo hilo kwa utaratibu huo Mjumbe aliekatazwa kusema jambo la utaratibu hatasimama kuendelea na maelezo yake mpaka Spika atakapokuwa ametoa kauli yake juu ya jambo hili la utaratibu iliotajwa. Nikushukuru Mhe. Spika, kwa kuniruhusu.

Nakuja katika 45 maelezo binafsi ya Mjumbe.

Mjumbe yoyote anaweza kwa kibali cha Spika kutoa maelezo yake binafsi katika wakati unaofaa kufuatana na mpangilio ya shughuli ambayo umewekwa kwa kanuni 27.

Kanunu ya 27(3) Mhe. Spika, shughuli za Kikao cha Baraza zitafanyika kwa utaratibu ufuatao kulingana na shughuli zitakazokuwepo katika haki hiyo.

Namba 3 Mhe. Spika, bila ya kuathiri masharti mengineyo kanuni hii kutakuwa na muda maalum kwa ajili ya Baraza kushughulikia hoja za Wajumbe ambao utakuwa ni siku moja katika Mkutano wa Kawaida wa Baraza na siku tatu katika Mkutano wa Bajeti ya mwaka ya Serikali.

Mhe. Spika, jambo ninalotaka kuzungumza ni dogo sana tu na jepesi sana roho ina sehemu yake na mimi sikuwahi kutolewa nyongo. Jana nilimuona Mhe. Mohammed Said Mohamed karibu mara mbili tatu hoja anafanikiwa na nimeona choyo kusema kweli kibinaadamu. Nimekuja karibu na hoja saba na zote zimekuwa zikipata kitanda.

Lakini wakati mwengine nashukuru viongozi wangu wakuu wananiita ndani tukaelezana na uongozi wako Mhe. Spika, na busara zako zimetusaidia sana hasa mimi kutuongoza hili na hili. Lakini mpaka leo Baraza linamalizika sijapa kauli yoyote na *hansard* hizi hapa Mheshimiwa nilichoambiwa nikilete na hichi chombo ni kizito.

Mhe. Spika, nafikiria Mhe. Jaku Hashim Ayoub tukubaliane naomba niisome *hansard*. Waziri na maelekezo yake ambayo ameyatoa hili jambo ni muhimu na muhimu kwetu sote. Mimi naunga mkono kabisa hoja yako lakini nafikiria kwamba vile vlile una uwezo wa kuleta hoja binafsi ili iwe na mshughulikiaji maalum. Mhe. Jaku Hashim Ayoub baada ya hapo nafikiri tuendelee. Ilikuwa bajeti hii.

Hoja hii ilikuwa ni hoja ya tarehe ya Kiislamu kwa muda mrefu na chombo hichi hichi kiliniahidi ni *hansard* hii na hichi chombo si masihara chombo kizito. Lakini sikuitwa hata kuambiwa kuwa kuna tatizo hili na mimi jana mwenzangu nimemuona kafanikiwa.

Mhe. Spika: Mhe. Jaku Hashim Ayoub naona nisikuache uendelee kwa sababu hoja hii nadhani ilitokezea katika Baraza lililopita lile lilijitokeza huko mimi sikuwepo wakati huo. Hivi sasa hivi umeileta Ofisini hili jambo halijaja humu ndani bado.

Kwa hiyo, siwezi kukuruhusu kuendelea nalo Mheshimiwa na tunaendelea na shughuli nyengine zinazofuata na kwa maana hiyo, kwa ufupi mchakato wa suala hilo hili suala limekuja Afisi kwa Spika na Spika, hajalileta ukumbini na mchakato wake ulikuwa haujamalika kwa sababu kuna maeneo ambayo lazima tuwasiliane niwasiliane na serikali lakini pia na chama chako kabla ya kulileta hilo suala lako humu ndani.

Kwa hiyo, naomba ufate huo utaratibu ukishakukamilika jambo lolote linalomuhusu Mjumbe litaingia ukumbini. Kwa hiyo, sitaki kukupa nafasi hiyo utumie muda huu sasa hivi kutaka kulileta kwa njia la kulilalamikia.

Tunaendelea baada ya hapo Waheshimiwa naomba kutoa matangazo machache ambayo yametufikia.

Kwanza ni tangazo la wageni Waheshimiwa mgeni aliepo ni mgeni mmoja mgeni wa Spika wa Baraza la Wawakilishi na Mgeni mwenyewe ni Mhe. Dkt. Abdalla Hasnuu Makame ambaye ni Mbunge kutoka Bunge la Afrika Mashariki. Karibu sana Dkt. Abdalla Hasnuu Makame. (*Makofi*)

Tangazo jengine ni tangazo la taarifa ya semina. Waheshimiwa Wajumbe tunaarifiwa kwamba kutakuwa na semina ya nusu siku leo siku ya Ijumaa kuanzia saa nane mchana katika ukumbi wetu wa juu. Semina hiyo ni kwa ajili ya kuwajengea uelewa Waheshimiwa Wajumbe kuhusiana na taasisi ya *ZDFCCM* inayojihusisha na mapambano ya maradhi ya *TB*, *HIV* na Malaria kwa udhamini wa *Global fund*.

Waheshimiwa Wajumbe tunaombwa kuhudhuria kwa wingi katika shughuli hiyo hapo saa nane mchana katika ukumbi wetu wa juu.

Tangazo jengine nililonalo Waheshimiwa linatoka kwa Mhe. Waziri wa Elimu na Mafuno ya Amali. Yeye anawatangazia Waheshimiwa Wawakilishi kwamba mnaalikwa rasmi kuhudhuria katika ufunguzi wa Tamasha la Michezo la Vyuo Vikuu *ZAHILFE CUP*. Leo tarehe 29/ 6/2018 katika Uwanja wa Amani saa tisa na nusu jioni, mgeni rasmi ni Mhe. Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar. (*Makofi*)

Kwa hiyo, Waheshimiwa kwa heshima na taadhima mnaombwa kuhudhuria kwa wingi ili kufanikisha ufumbuzi huo na kusaidia kuona vipaji vya vijana wetu. Ahsanteni sana.

Kwa hiyo, kidogo itagongana na semina lakini nafikiri baadae mnaweza mkalipanga na likakaa sawa hili.

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Kuweka Masharti Bora ya Usimamizi wa Mahakama kufanunua Utumishi wa Mahakama kuanzisha Afisi za Mtendaji Mkuu wa Mahakama na Mrajisi, Kuanzisha Mfuko wa Mahakama na kuweka Mashati mengine yanayohusiana na hayo.

(Kusomwa kwa mara ya Kwanza)

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi (Kny. Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora naomba utoaji wa Mswada wa Sheria ya Kuweka Masharti Bora ya Usimamizi wa Mahakama, kufafanua Utumishi wa Mahakama, kuanzisha Afisi ya Mtendaji Mkuu wa Mahakama na Mrajisi, kuanzisha Mfuko wa Mahakama na kuweka masharti mengine kuhusiana na hayo. Naomba kusomwa kwa mara ya kwanza. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mswada wa Sheria kuanzisha Afisi ya Mkaguzi wa Mkuu wa Elimu na kuweka Masharti ya Ukaguzi ya Elimu pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

(Kusomwa kwa mara ya Kwanza)

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kusoma Mswada wa Sheria wa kuanzisha Afisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu na kuweka Masharti ya Ukaguzi wa Elimu pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo kusomwa kwa mara ya kwanza Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar na kuweka Masharti Bora yanayohusiana na Kazi, Uwezo, Uongozi na Mambo mengine yanayohusiana na hayo.

(Kusoma kwa mara ya Kwanza)

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais (kny) Mhe. Waziri wa Bahari, Utalii na Mambo ya Kale: Mhe. Spika, kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Bahari, Utalii na Mambo ya Kale naomba kutoa hoja Mswada wa Sheria kuanzisha Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanazibar na kuweka Masharti Bora yanayohusiana na kazi, Uwezo, Uongozi na mambo mengine yanayohusiana na hayo kusomwa kwa mara ya kwanza. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kwa mujibu wa taarifa ni kwamba shughuli zote ambazo zimepangwa katika Mkutano wetu huu wa bajeti itakuwa zimekamilika baada ya

Miswada ya Sheria hiyo ambayo imesomwa kwa mara ya kwanza ambayo tunategemea itasomwa kwa mara ya pili katika kikao kinachofuata.

Kwa maana hiyo sasa naomba nichukuwe nafasi hii kwa heshima na taadhima nimkaribishe Mhe. Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar ili aweze kuja kutufungia Baraza. Karibu Mheshimiwa. (*Makofi*)

KUAKHIRISHA BARAZA

Mhe. Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwanza kabisa hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, Mwenye wingi wa rehma, Muumba mbingu na ardhi na vilivyomo ndani yake kwa kutujaalia uhai na afya njema na kutuwezesha kufanikisha Mkutano huu wa Kumi wa Baraza la Tisa ulioanza tarehe 09 Mei, 2018. Ninafuraha kuona kwamba shughuli zote zilizopangwa katika ratiba ya Mkutano huu zimekamilika kwa wakati na kwa ufanisi mkubwa wa kupigiwa mfano.

x

Mhe. Spika, Kwa mara nyengine tena tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kuiweka nchi yetu katika hali ya amani, utulivu, umoja, upendo na mshikamano mkubwa miongoni mwa wananchi wetu. Hali hii imetuwezesha sisi viongozi na wananchi kutekeleza majukumu yetu ya kiuchumi na kijamii kwa ufanisi jambo ambalo limechangia kuimarisha uchumi na ustawi wa nchi yetu. Hivyo, sote hatuna budi kuhakikisha kuwa tunaisimamia, tunailinda na kuidumisha hali hii kwa mustakbali wa nchi yetu na wananchi wake.

Mhe. Spika, kwa umuhimu na uzito wa kipekee napenda kumpongeza kwa dhati Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Ali Mohammed Shein, kwa miongozo yake mbali mbali ya busara na hekima anayoitoa kwetu inayotuwezesha kusimamia vyema majukumu tunayopangiwa ya kuiendesha Serikali yetu. Kwa hakika, Dkt. Ali Mohammed Shein ni dira yetu ya matumaini katika kujenga uchumi imara ambao unaoimarika kila mwaka na kuleta tija kwa wananchi ambao unatokana na usimamizi na utekelezaji bora wa Ilani yetu ya CCM ya mwaka 2015 - 2020. Mafanikio haya tumeyapata kutokana na nia yake thabiti kwa wananchi wake. Nampongeza sana Rais wetu kwa juhudi zake na kuona mbali katika kuiletea nchi yetu maendeleo endelevu.(*Makofi*)

Mhe. Spika, vile vile, napenda kutoa pongezi zangu kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa namna anavyosimamia utekelezaji wa majukumu yake ya kuiongoza nchi yetu. Aidha, nampongeza kwa dhati namna anavyokisimamia na kukiongoza Chama chetu cha Mapinduzi na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sote ni mashahidi wa jinsi alivyoweza kurudisha nidhamu ya utendaji kazi, kuondoa ubadhirifu wa mali za umma na kuwezesha wananchi wa Tanzania kufaidika kwa pamoja na rasilimali za nchi na kupata huduma za kijamii ipasavyo. Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli hongera sana.(*Makofi*)

Mhe. Spika, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru na kukupongeza wewe Mheshimiwa Spika pamoja na Naibu wako, Mhe. Mgeni Hassan Juma, Wenyeviti wa Baraza, Katibu wa Baraza na Watendaji wote wa Baraza la Wawakilishi kwa kuliendesha Baraza letu kwa umahiri na ufanisi mkubwa. Mmefanya kazi kubwa katika kipindi hiki cha Baraza la Bajeti ambalo lilikuwa na mambo mengi. Naamini busara zako pamoja na viongozi wenzako zimechangia kwa kiasi kikubwa kufanikisha mkutano huu ambao leo tunafikia tamati.(*Makofi*)

Mhe. Spika, pia, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wenzangu wa Baraza la Wawakilishi kwa kutumia haki yao ya Kikatiba na Kidemokrasia kwa kuchangia na kuuliza maswali mbali mbali ambayo Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu Mawaziri wamejitahidi kuyapatia ufafanuzi wa kina. Nawashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu Mawaziri kwa kazi mlioifanya ya kuwaelewesha Waheshimiwa Wajumbe na wananchi wetu kwa ujumla.

Mhe. Spika leo ni siku ambayo tunahitimisha mkutano wetu huu mrefu wa bajeti ambao umemalizika salama, katika Mkutano huu wa Kumi wa Baraza la Tisa tulijadili na kupitisha Bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Waheshimiwa Wajumbe walipata nafasi ya kuzichangia kwa umahiri, uweledi na uwazi bajeti zote za Kisekta na kuzipitisha. Kadhalika, kwa umoja wetu tuliweza kuipitisha Bajeti Kuu ya Serikali ya mwaka 2018/2019, jambo ambalo litaiwezesha Serikali yetu kutekeleza mipango yake ya kimaendeleo iliyojipangia kwa ufanisi mkubwa.

Mhe. Spika, napenda kutoa ombi langu kwa Waheshimiwa Wajumbe wenzangu pale mtakapogundua kuwa mipango tuliyoipanga katika Baraza letu hili Tukufu haiendi kama tulivyokubaliana naomba msisite kuishauri Serikali hata kabla ya muda wa kikao cha Baraza hakijafikia kwani kuna vikao vyetu halali ambavyo vina uwezo wa kuufanyia kazi ushauri huo.

Mhe. Spika, Mkutano huu pia umejadili Miswada Miwili (2) na kuipitisha kuwa Sheria. Miswada yenyewe ni:-

(i) Mswada wa Sheria ya Matumizi *(Appropriation Bill*); na
(ii) Mswada wa Sheria ya Fedha (*Finance Bill*).

Hata hivyo Miswada ifuatayo imesomwa kwa mara ya kwanza:-

(i) Mswada wa Sheria ya Wakala wa Uchapaji;
(ii) Mswada wa Sheria ya Usimamizi wa Mahkama;
(iii) Mswada wa Sheria ya kuanzisha Ofisi ya Ukaguzi wa Elimu Zanzibar.

Aidha, katika Mkutano huu jumla ya maswali ya msingi 205 na maswali ya nyongeza 464 yaliulizwa na kupatiwa ufafanuzi wa kina na Waheshimiwa Mawaziri. Kuna maswali mengine yaliyoahidiwa kujibiwa kwa maandishi kutokana na sababu mbali mbali. Napenda kuwathibitishia Waheshimiwa Wajumbe kuwa maswali yote ya nyongeza

ambayo yameahidiwa kujibiwa kwa maandishi, majibu yake yatafikishwa kwenu kwa muda muafaka.

Mhe. Spika, hali ya upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama Zanzibar ni ya kuridhisha. Upatikanaji wa maji umefikia asilimia 62 ya mahitaji ya wananchi. Bado kuna asilimia 38 ya wananchi wetu ambao wanaendelea kusumbuka na huduma ya maji safi na salama. Hali hii inatokana na kuongezeka kwa idadi ya watu, uchakavu wa miundombinu ya maji na kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi na kijamii mijini na vijijini kunakopelekea kutokuwepo kwa uwiano kati ya maji yanayozalishwa na mahitaji halisi. Ili kukabiliana na tatizo hilo, Serikali kupitia Mamlaka ya Maji (*ZAWA*) inaendelea kutekeleza miradi 7 ya maji chini ya Programu Kuu mbili ya Uhuishaji na Upanuzi wa Shughuli za Maji Mijini na Programu ya Usambazaji Maji Vijijini. Programu hizo zina lengo la ujenzi wa matangi, ujenzi wa majengo ya mitambo ya kutibu maji, uchimbaji na uendelezaji wa visima, ulazaji wa mabomba mapya, kudhibiti upotevu wa maji pamoja na ukarabati wa miundombinu ya maji. Juhudi hizi zinafanywa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikiana na wananchi pamoja na Washirika wetu wa Maendeleo.

Mhe. Spika, napenda kutoa wito kwa wananchi wanaopata huduma ya maji kuchangia huduma hii ili Serikali ipate nguvu ya kuendelea kutoa huduma kwa wananchi wengine wenye upungufu wa maji katika maeneo yao. Sambamba na juhudi hizo, Serikali inaendelea kuwapatia maji wananchi wake wenye ukosefu wa huduma hii kupitia magari maalum ili kuwaondolea usumbufu wa kutafuta huduma ya maji safi na salama masafa marefu. Ninawaomba wananchi waendelee kuwa wastahamilivu kwa wale wanaopata usumbufu wa maji kwani Serikali inaendelea na juhudi za kulipatia ufumbuzi suala hilo. Sambamba na hilo, napenda kumpongeza Mkurugenzi Mkuu wa *ZAWA*, Ndugu Mussa Ramadhan Haji kwa juhudi yake ya kuwapatia maji safi na salama kwa kiwango kikubwa katika muda mfupi baada ya uteuzi wake. Ni matumaini yangu kwamba utaziendeleza juhudi zake hizo.(*Makofi*)

Mhe. Spika, suala la uuzaji wa ardhi bila ya kufuata sheria limekuwa likiibua mizozo mingi katika nchi yetu. Kwa bahati mbaya uuzaji huu wa ardhi umekuwa ukichangiwa na baadhi ya watendaji wa Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati na baadhi ya Masheha wetu. Jambo hili halikubaliki na wale wote wanaojishughulisha na vitendo hivi watachukuliwa hatua za kisheria. Natoa agizo kwa Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya kuwafichua Masheha wanaoendeleza tamaa zao za kuuza maeneo ya ardhi bila ya kufuata sheria, hatua kali zichukuliwe pamoja na kuachishwa Usheha.

Ni vyema wananchi wakaelewa kuwa mara tu baada ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ya Januari, 1964, ardhi yote imewekwa chini ya mamlaka ya Serikali, hivyo ardhi ni mali ya Serikali na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, ndie msimamizi mkuu. Kwa hivyo kuuza mali ya Serikali bila ya idhini yake tafsiri yake ni wizi wa mali ya umma. Natoa wito kwa wananchi wote kujiepusha na tabia hii ya kuuza ardhi kwani jambo hili ni kosa kisheria. Hivyo, Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati ndio yenye mamlaka ya kutoa ardhi kisheria kwa idhini ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein na sio mtu au Taasisi nyengine yoyote nchini.

Mhe. Spika, katika msimu uliopita wa mvua za Masika zilizoambatana na upepo mkali, Zanzibar kama sehemu nyengine za Afrika Mashariki ilikumbwa na mvua kubwa zilizosababisha athari mbali mbali ikiwa pamoja na vifo vya watoto wanne (4), uharibifu mkubwa wa miundombinu hasa barabara na makaazi ya watu. Katika kuwafariji wananchi wake, Serikali imetoa ubani kwa wafiwa na kuwasaidia baadhi ya wananchi waliopatwa na maafa kwa kuwapa msaada wa chakula pamoja na baadhi ya vifaa vya ujenzi. Aidha, Serikali inaendelea na juhudi za kurekebisha athari zilizotokea hasa za ukarabati wa barabara katika maeneo mbali mbali nchini.

Mhe. Spika, napenda kuchukuwa fursa hii kutoa pole kwa wananchi wote waliopatwa na maafa katika maeneo mbali mbali ya visiwa vyetu Unguja na Pemba. Hata hivyo, kwa mara nyengine tena Serikali inaendelea kutoa wito kwa wananchi kujihadhari na majanga kwa kuepuka ujenzi holela pia kutokujenga katika maeneo hatarishi yakiwemo mabonde na njia asili za maji pamoja na kuepuka kulaza mabati katika nyumba zetu ili kupunguza maafa yanayosababishwa na mvua na upepo hapa visiwani kwetu. Nawapongeza wananchi kwa juhudi za awali walizozichukua za kuzibua mashimo na kujenga mitaro ili kuepuka mkusanyiko wa maji na kuweza kupita kirahisi. Hongereni sana wananchi kwa juhudi mlizozichukua.

Mhe. Spika, kama tunavyojua kwamba vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto unaendelea kuwa kero kubwa katika nchi yetu. Ili kukabiliana na vitendo hivyo, Serikali imeandaa Mpango kazi wa Kitaifa wa Kupambana na Vitendo vya Ukatili na Udhalilishaji wa Wanawake na Watoto. Mpango huu maalum wa miaka 5 (2017 - 2022) ambao utaongeza juhudi za kupambana na kadhia hii. Sambamba na mpango huo, Serikali imezifanyia marekebisho baadhi ya Sheria zinazohusiana na udhalilishaji na ukatili wa wanawake na watoto ikiwemo Sheria ya Makosa ya Jinai Nam. 6 ya mwaka 2018 na Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai ya Nam. 7 ya mwaka 2018, ili kuhakikisha kuwa watendaji wa makosa hayo wanapata adhabu inayostahiki ili kupunguza na kuyaondoa kabisa matendo hayo mabaya yanayotia aibu nchi yetu, pamoja na kutoa haki kwa waathirika wa vitendo vya udhalilishaji. Sheria hizo tayari zimeshasainiwa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ambazo zinatoa adhabu kali, pamoja na kuondoa dhamana kwa watuhumiwa wa vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia.

Mhe. Spika, Sheria hizo zimeziongezea nguvu Mahkama za Wilaya na Mikoa za kuweza kutoa adhabu kali zaidi kwa waliotiwa hatiani. Waheshimiwa Wajumbe wenzangu, taasisi zinazohusika, wazee, walezi na wananchi wote, napenda kuchukuwa fursa hii kutoa wito kwenu tuendelee kushirikiana kwa hali na mali katika kupambana na kadhia hii. Aidha, nawanasihi wazee wenzangu kuwa linapotokea tukio la udhalilishaji katika familia zetu tuache tabia ya kumaliza masuala haya kienyeji na kuondoa muhali ili sheria iweze kuchukua mkondo wake, vyenginevyo ni kudhoofisha juhudi za serikali katika kupambana na vitendo hivyo. Imani yangu kuwa tukishirikiana kwa pamoja suala la udhalilishaji litabakia kuwa historia, wananchi watakuwa na amani na vizazi vyetu vitajengeka kitabia na kuwa na maadili mema. Naomba tushirikiane kwani “Umoja ni Nguvu na Umoja ni Ushindi”.

Napenda kuwakukumbusha wananchi maneno aliyosema Mhe. Rais Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi wakati akilihutubia Baraza la Eid El Fitri tarehe 15 Juni, 2018, alisema; nanukuu.

> "Napenda kuwaasa wazazi na walezi kwamba linapotokezea kosa la udhalilishaji ambalo limefanywa na mtu wa familia, hatupaswi kabisa kulitolea hukumu au kulimaliza kifamilia. Tunapoamua kuyamaliza matatizo haya kifamilia au kuchelea kutoa ushahidi sahihi katika vyombo vya sheria, inakuwa ni sawa na kudhoofisha jitihada za serikali na kuyaendeleza maovu." Mwisho wa kunukuu.

Hivyo, nawasisitiza wananchi kuwa mtu yeyote ambae atamkingia kifua mdhalilishaji na yeye atachukuliwa kuwa ni mdhalilishaji na hatua kali dhidi yake zitachukuliwa.

Mhe. Spika, katika kupambana na usafirishaji, uingizaji, usambazaji na utumiaji wa dawa za kulevya Zanzibar, serikali kupitia Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Kudhibiti Dawa za Kulevya inaendelea na kazi ya kusimamia na kuratibu mapambano dhidi ya dawa hizo. Pia, tume inaratibu utekelezaji wa Sheria ya Dawa za Kulevya Zanzibar. Katika utekelezaji wake imefanya mafunzo kwa Mahakimu wa Mikoa na Wilaya za Mahkama za Zanzibar, Jeshi la Polisi, Waendesha Mashtaka, na Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi juu ya Sheria ya Dawa za Kulevya ili waweze kuielewa na kuitekeleza ipasavyo Sheria hiyo. Aidha, tume inaendelea kutoa elimu ya kinga dhidi ya matumizi ya dawa za kulevya kwa lengo la kuwaokoa vijana wetu na matumizi ya dawa hizi. Vile vile, tume inaendelea na utekelezaji wa mpango wa tiba na marekebisho ya tabia kwa waathirika wa matumzi ya dawa za kulevya kwa kushirikiana na taasisi mbali mbali na jamii kwa ujumla.

Mhe. Spika, tume kwa kushirikiana na wadau wa udhibiti wa dawa za kulevya imeandaa mkakati wa kuhakikisha kuwa kesi zote za dawa za kulevya zinawasilishwa Mahkamani haraka, ili kuhakikisha kwamba kesi hizo zinapata ufumbuzi wa haraka na kuepusha kuharibiwa kwa ushahidi. Pia, tume imeshaanza kazi ya uangamizaji wa dawa za kulevya pamoja na kuyafanyia kazi maeneo makorofi ya dawa za kulevya kwa kuliwezesha Jeshi la Polisi kushirikiana na Kamati za Ulinzi na Usalama za Mikoa dhidi ya mapambano na kurudisha heshima ya nchi yetu. Hata hivyo, juhudi za pamoja bado zinahitajika. Naiomba jamii isichoke tuendelee kutoa taaluma kwa vijana wetu juu ya athari za dawa hizo ili kuwaokoa vijana wetu ambao ndio nguvu kazi ya Taifa letu.

Mhe. Spika, Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi (*ZAECA*) inaendelea na kazi ya kuelimisha jamii juu ya athari za rushwa na uhujumu uchumi nchini. Mamlaka imetoa elimu kwa wananchi kupitia mikutano ya hadhara pamoja na skuli tofauti za Unguja na Pemba, vipindi vya redio na televisheni pamoja na machapisho mbali mbali. Vile vile, Mamlaka imefanikiwa kufunga mitambo kwa ajili ya programu ya kupiga simu namba ya bure ambayo ni 113. Madhumuni ya huduma hii ni kurahisisha kutoa taarifa ya vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi. Tayari mafanikio ya utumiaji programu ya kupiga simu yameanza kuonekana kwani wananchi wengi wamepata ari na utayari wa kuripoti matukio ya rushwa na uhujumu wa uchumi. Napenda kutoa wito kwa wananchi

kuendelea kuitumia namba hii kuyaripoti matukio ya vitendo vya rushwa ili hatua za haraka ziweze kuchukuliwa.

Mhe. Spika, Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi imezindua Mkakati Jumuishi wa Kitaifa wa Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi. Lengo la Mkakati huu ni kuishirikisha jamii katika mapambano dhidi ya rushwa. Sambamba na mkakati huo, mamlaka inaendelea kufanya kazi ya udhibiti wa vitendo vya rushwa na uhujumu wa uchumi katika taasisi na idara mbalimbali za serikali. Udhibiti huo umepelekea mamlaka kuokoa jumla ya shilingi 169,028,120/=. Lengo la udhibiti huo ni kuweza kuzuia upotevu wa mapato ya serikali na kupunguza vitendo vya rushwa katika utoaji wa huduma kwa wananchi bila ya pingamizi zozote, na bila ubaguzi wa aina yoyote.

Mhe. Spika, hali ya usalama barabarani nchini ni tishio kwa jamii kutokana na uendeshaji ovyo wa vyombo vya moto. Vijana wajulikanao kama T1 bado hawajadhibitiwa ipasavyo. Kadhalika alama za usalama barabarani bado hazijafuatwa na madereva walio wengi. Mambo yote haya yanachangia kwa kiasi kikubwa kutokea kwa ajali za mara kwa mara katika barabara zetu, jambo ambalo hupelekea kuwasababishia wananchi kupata ulemavu au vifo. Kutokana na hali hiyo, serikali hairidhishwi hata kidogo na hali ya usalama barabarani.

Mhe. Spika, naliagiza Jeshi la Polisi na idara zinazohusika na vyombo vya moto kushughulikia ipasavyo usalama wa barabarani kwa kufanya kazi zao kwa uadilifu ili kuokoa maisha ya wananchi wetu na vyombo vyao. Hivyo, madereva wote wahakikishe kuwa wanafuata sheria za usalama barabarani na kupunguza mwendo kasi katika maeneo ya makaazi ya watu, yakiwemo skuli na hospitali, ili watu wetu watembee barabarani wakiwa katika hali ya amani. Inasisitizwa pia waendesha vyombo vya moto vya magurudumu mawili wafuate sheria ya kuvaa kofia ngumu, ili kuokoa maisha yao pindipo wakipata ajali. Kutokufanya hivyo ni kuvunja sheria.

Mhe. Spika, itakumbukwa kuwa kila ifikapo tarehe 05 Juni ya kila mwaka huwa tunaadhimisha Siku ya Mazingira Duniani. Kwa mwaka huu wa 2018, kaulimbiu ya maadhimisho hayo ni “Pambana na Uchafuzi wa Mazingira kwa kukabiliana na takataka za Plastiki” (*Beat Plastic Pollution*). Katika kuadhimisha siku hii, Ofisi yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali zimeanzisha Kampeni Maalum ya Usafi na Utunzaji wa Mazingira katika Skuli za Msingi na Sekondari kwa Unguja na Pemba. Lengo kuu la kuanzisha kampeni hiyo ni kujenga utamaduni wa kutunza na kuhifadhi mazingira miongoni mwa watoto wetu tangu wakiwa wadogo kwani kama wasemavyo wahenga, ‘mtoto umleavyo ndivyo akuavyo’ na ‘udongo upate ulimaji‘.

Mhe. Spika, napenda kuzipongeza taasisi zote za serikali na za watu binafsi pamoja na wananchi wote walioshiriki katika shughuli mbali mbali za uhifadhi wa mazingira, kwa kufanya usafi na upandaji wa miti ikiwemo miche ya mikarafuu, matunda na viungo ambayo jumla ya miche 3,910,401 ilipandwa kwa Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, kwa upande wa misitu, jumla ya hekta 116 za mashamba na hifadhi za serikali zimepandwa miti katika msimu huu. Misitu ya jamii hekta 383, mashimo ya

mchanga hekta 6 na kando mwa bahari hekta 56. Haya ni mafanikio makubwa katika kuhifadhi mazingira yetu. Hata hivyo, natoa wito kwa wananchi tuitunze miti hii iliyopandwa ili ikuwe na kuleta manufaa kwetu na vizazi vijavyo.

Mhe. Spika, hali ya uzalishaji na upatikanaji wa chakula nchini imeendelea kuimarika katika msimu wa 2017/2018. Uzalishaji wa chakula kwa ujumla umefikia tani 357,932 ukilinganisha na mahitaji ya tani 583,651 ya chakula kwa sasa. Kutokana na uzalishaji huo, hivi sasa Zanzibar inajitosheleza kwa chakula kwa asilimia 61 ukilinganisha na asilimia 42 iliyorekodiwa kwa mwaka 2016. Mafanikio haya yanatokana na kuwepo kwa hali nzuri ya hewa iliyopelekea uzalishaji kuwa mzuri na kuimarika kwa mazao ya mpunga, muhogo, ndizi, viazi vitamu, mahindi, mboga na matunda. Kadhalika, serikali inajitahidi kutoa ruzuku kwa wakulima kwa kushirikiana na taasisi zisizo za kiserikali katika kuunga mkono juhudi za kuongeza uzalishaji kwa kutoa taaluma ya kilimo cha kisasa na matumizi bora ya teknolojia, ambayo yamechangia kwa kiwango kikubwa upatikanaji wa chakula cha kutosha nchini.

Mhe. Spika, wakati wa uwasilishaji wa Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Waheshimiwa Wajumbe wameonesha kutokuridhishwa kwao na kiwango cha ujenzi wa skuli za Serikali zilizojengwa na zinazoendelea kujengwa nchini. Serikali kwa upande wake imeridhia kuundwa kwa Kamati Teule ya kuchunguza suala hili. Naomba kuisisitiza Kamati hiyo kufanya kazi zake kwa uaminifu na uadilifu mkubwa kwa maslahi ya nchi yetu. Pia, Serikali inaahidi kuifanyia kazi taarifa itakayowasilishwa na Kamati hiyo kwa kuwachukulia hatua za kisheria watu wote watakaobainika au watakaohusika na ubadhirifu au kadhia hiyo ya ujenzi huo wa kiwango cha chini ambao umeipotezea fedha nyingi Serikali yetu na kuhujumu uchumi wetu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, uchumi wa Zanzibar unaendelea kuimarika na kukua siku hadi siku, hali hii inatokana na ukusanyaji mzuri wa mapato na kuzuia uvujaji wa mianya ya mapato hayo, kama yalivyokwisha elezewa kwa ufasaha na kwa undani na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango.

Mafanikio haya yameiwezesha Serikali kutekeleza majukumu yake kwa uhakika kama ilivyojipangia. Naamini kwamba, Bajeti ya mwaka 2018/2019 ambayo tumeipitisha hivi punde na kwa uongozi imara na mahiri wa Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein tutaitekeleza kwa asilimia mia moja na kuleta manufaa kwa wananchi wetu. Nia ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuondoa utegemezi katika Bajeti yetu. Mengi yameelezwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango wakati akiwasilisha hotuba ya Bajeti kwa mwaka wa fedha wa 2018/2019.

Mhe. Spika, kufuatia hoja binafsi iliyowasilishwa na Mhe. Mohammed Said Dimwa aliwasilisha kwa umahiri na uzalendo tumeipokea pamoja na maazimio yote yaliyowasilishwa Barazani. Naahidi yatafanyiwa kazi kwa mujibu wa sheria na taratibu kwani serikali inaendelea kuchukuwa hatua na kulifuatilia suala hilo, kwani vitendo vilivyofanyika ni kuitia aibu nchi yetu.

Mhe. Spika, nawaomba Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na wananchi watambue kuwa serikali yetu ina Vijana wenye uwezo mkubwa wa kuingia katika mashindano haya na kufanikisha azma ya nchi yetu, bila ya kufanya udanganyifu wa aina yoyote tunakuhakikishieni kwa serikali itakuwa makini kwa vyombo vinavyohusika na maandalizi ya vijana wetu ili kuepuka vitendo vinavyo kwenda kinyume na taratibu za michezo za Kitaifa na Kimataifa.

Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena napenda kuwashukuru wale wote waliotuwezesha kukamilisha shughuli zilizopangwa kwenye Mkutano huu kwa ufanisi mkubwa na mshikamano mkubwa. Pongezi hizo pia ziwafikie watendaji wote wa Baraza hili la Wawakilishi wakiongozwa na Katibu wa Baraza, Ndugu Raya Issa Msellem. Vile vile, nawapongeza wakalimani wetu wa lugha ya alama ambao wamewawezesha Waheshimiwa Wawakilishi na wananchi wenye ulemavu wa kusikia kufuatilia yote yaliyokuwa yakiendelea ndani ya Baraza lako Tukufu. Hali kadhalika, navishukuru vyombo vyote vya habari vilivyoshiriki kikamilifu katika mkutano huu kwa kuwapatia wananchi taarifa juu ya mwenendo mzima wa majadiliano na Wajumbe yaliyokuwa yakiendelea hapa Barazani.

Mhe. Spika, kwa kumalizia niwatakie Waheshimiwa Wawakilishi kila la kheri na mafanikio mema katika kuwatumikia wananchi wao Majimboni mwao na utekelezaji wa ahadi zao na Ilani ya CCM ya mwaka 2015 – 2020 kwa vitendo. Pia, nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kukamilisha vyema funga ya Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, ambapo Mtume wetu Muhammad (SAW) amesema “mwanzo wa mwezi wa Ramadhani ni Rehma, katikati yake ni Msamaha na mwisho wake ni Kuachwa Huru na moto”, imani na mafunzo hayo yamepelekea kusherehekea Sikukuu ya Eid el Fitri kwa salama, amani na utulivu mkubwa. Pia, tuliyojifunza katika mwezi huo Mtukufu wa Ramadhan tuendelee kuyatekeleza. Huku tukimuomba Mwenyezi Mungu atuongoze katika njia iliyonyooka, njia ya wale walioneemeshwa sio ya wale waliokasirikiwa au ya wale walioghadhibikiwa na pia kuendeleza amani na utulivu wa nchi yetu. Aidha, ninawatakia Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu wote safari njema na mrudi salama Majimboni mwenu na hasa wale Wajumbe wenzetu wanaokwenda Pemba.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, naomba sasa kwa heshima na taadhima kutoa hoja kwamba, Baraza lako Tukufu liahirishwe hadi siku ya Jumatano tarehe 19 Septemba, 2018 saa 3.00 barabara za asubuhi Mwenyezi Mungu akitujaalia.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, hoja imetolewa na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais na hoja yenyewe ni kwamba, Baraza hili liakhirishwe mpaka siku ya Jumatano tarehe 19 September, 2018 saa 3:00 barabara za asubuhi. Sasa naomba niwahoji wale wote wanaounga mkono hoja hiyo wanyanyue mikono yao. Wanaokataa, waliokubali inaonesha wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Kwanza kabisa nitowe shukurani zangu za dhati kabisa kwa Mhe. Makao wa Pili wa Rais, kwa hotuba yake nzuri ameitoa hapo na khatimae kuweza kutoa hoja ya kuakhirishwa kwa Baraza. Sasa kabla sijafanya hiyo shughuli ya kuakhirisha nina tangazo moja, tangazo hili litatoka kwa Mhe. Waziri wa Kilimo.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, anawatangazia Waheshimiwa wajumbe kwamba kutakuwa na shughuli ya Uzinduzi wa kuvuna Mpunga Kitaifa huko Kibokwa na Mgeni rasmi katika zoezi hilo ambalo linafanyika katika Mkoa wa Kaskazini, Wilaya ya Kaskazini A, atakuwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, na kwa umuhimu wa shughuli hiyo ameliomba Baraza kupitia mimi hapa Spika na Kamati ya Kudumu ya Fedha Biashara na Kilimo, kwamba niwaatarifu wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi wahudhurie zoezi hilo ambalo litafanyika siku ya tarehe 1 Julai, 2018 siku ya Jumapili na wanatakiwa wafike pale saa 2:00 asubuhi kwa vile Mgeni Rasmi Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi atafanya uzinduzi huo saa 3:00 asubuhi. Twende huko ili kuona matokeo ya Kilimo cha Mpunga wa umwagiliaji na shadidi unaoleta tija kwa kuwa na mavuno makubwa kwa eneo dogo na kumnufaisha Mkulima.

Waheshimiwa wajumbe, hilo ndio Tangazo letu kutoka kwa Mhe. Waziri wa Kilimo, Mhe. Mwalimu Rashid Ali Juma, sasa baada ya tangazo hilo. Naomba sasa kabla sijaakhirisha shughuli za Baraza kama hoja iliyotolewa naomba sate tunyanyuke kwa ajili ya wimbo wa Taifa.

WIMBO WA TAIFA

Mhe. Spika: Sasa naomba niakhirishe shughuli za Baraza la Wawakilishi mpaka siku ya Jumatano tarehe 19 Septemba, 2018 saa 3.00 barabara za asubuhi.

(Saa 4:50 Baraza liliakhirishwa mpaka tarehe 19 Septemba, 2018 saa 3:00 asubuhi)